

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

12 JUNI, 2018



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – TAREHE 12 JUNI, 2018

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**415. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa barabara pembezoni mwa Ziwa Nyasa, hususan Wilaya ya Ludewa na Mkoa wa Njombe; eneo hilo lenye urefu wa km 150 hutegemea usafiri wa Meli ambao hauna tija kwa Wananchi walio wengi:-

- (a) Je, Serikali itawasaidia vipi Wananchi wa maeneo hayo yenyewe Vijiji 22 kupata barabara ya uhakika;
- (b) Kwa kuwa Wananchi wameanza kutengeneza wenyewe barabara kwa

nguvu zao; Je, Serikali inatoa tamko gani la kuunga mkono juhudhi hizo za Wananchi.

#### **416. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Rais wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika kampeni za uchaguzi tarehe 18/11/2005 aliwaahidi Wananchi wa Kibiti kuwa Serikali yake itajenga barabara ya Kibiti – Kikale ili kupunguza adha kubwa ya usafiri wanayopata Wananchi wa Vijiji vya Mchukwi, Rungungu, Nyamatanga na Kikale ambamo barabara hiyo inapita:-

- (a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza;
- (b) Je, ujenzi huo unaotarajiwa utakuwa ni wa kiwango gani.

#### **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

#### **417. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali ilianzisha Wakala wa Misitu (TFS) kwa lengo la kuhifadhi Misitu, kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali ya Misitu:-

Je, ni kwa kiasi gani Maafisa wa Misitu walioko Mikoani, Wilayani wameweza kuokoa Misitu inayozidi kuteketea hapa nchini.

#### **418. MHESHIMIWA HASNA SUDI KATUNDA MWILIMA (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wananchi wa Humule, Ubanda, Tandala na maeneo mengine ya Itebula wamekuwa wakikosa maeneo ya kulima kwa madai kuwa wanaingilia maeneo ya Hifadhi:-

- (a) Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kusogeza mipaka kwa kushirikiana na TAMISEMI ili Wananchi wapate maeneo ya kulima;
- (b) Je, ni lini Serikali itamaliza usumbufu wanaoupara Wananchi wa Kijiji cha Kalilani kwa kudaiwa kuwa wamo ndani ya Hifadhi wakati Kijiji hiki kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria.

#### **419. MHESHIMIWA RHOA EDWARD KUNCHELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Hifadhi na Wananchi katika Kata ya Kapalambsenga, Isengule na Ikola;

(b) Kwa kuwa migogoro hiyo imechukua muda mrefu bila suluhu hivyo kusababisha usumbufu na hasara kwa Wananchi, Je, Serikali haioni kuwa migogoro hiyo imesababisha umasikini mkubwa kwa Wananchi kushindwa kuendeleza shughuli za kiuchumi kwenye maeneo yao hivyo ifanye haraka kutafuta ufumbuzi.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**420. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Vijana na Akina Mama wengi kwa sasa wamewekeza katika kilimo cha mbogamboga, lakini wanakabiliwa na Changamoto kubwa ya ukosefu wa masoko ya uhakika kwa bidhaa zao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Wakulima hao kupata soko la uhakika la bidhaa zao.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **421. MHESHIMIWA SUSANNE PETER MASELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wananchi wakazi wa Kijiji cha Ishokelahela Misungwi Mwanza wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya kihalifu, kinyama na kikatili na vyombo vya Dola kwa kuwaondoa katika makazi yao na kuacha kuchimba dhahabu ili eneo hilo libaki kwa Mwekezaji anayetaka kuwaondoa kwa nguvu kinyume cha Sheria.


- (a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu vitendo hivyo wanavyofanyiwa Wananchi hao;
- (b) Je, Serikali iko tayari kuunda timu kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mgogoro huo na kuchukua hatua stahiki ambazo zitamaliza kabisa mgogoro na kuwajibisha wote ambao wamesababisha hali iliyopo sasa.

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

### **422. MHESHIMIWA OMARY TEBWETA MGUMBA (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Ubena,

Ngerengere hadi Mvuha yenyeye urefu wa zaidi ya km 70 inaunganisha Wilaya ya Bagamoyo na Halmashauri ya Morogoro ambako Makao Makuu ya Wilaya mpya Mvuha yanatarajiwa kujengwa. Aidha, barabara hii pia inaunganisha Mkoa wa Pwani na Morogoro. Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro haina uwezo wa kuhudumia barabara hiyo:-

- 
- (a) Je, ni lini Serikali itakubali ombi la kupandisha barabara hiyo kuwa ya Mkoa;
  - (b) Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo ya Ubena – Mvuha kwa kiwango cha changarawe ili kuitika mwaka mzima.

#### **423. MHESHIMIWA ENG. RAMO MATALA MAKANI (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Uwanja wa Ndege mbadala katika Mji wa Tunduru baada ya uwanja uliokuwepo awali kuhamishwa kutoka katikati ya Mji.

**DODOMA**  
**12 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**